KUMKUMBUKA BWANA

Asante, Ndugu Neville. Nina furaha sana kuwa hapa, Ndugu Neville, na fu—fursa ya kuketi katika ulimwengu huu wa Roho tena, katika Kristo Yesu. Wala idadi kamwe haijapata kunisumbua, hunichochea daima. Unajua, zaidi... Mimi niko nyumbani zaidi wakati nikiwa na idadi ndogo, maana hivyo ndivyo ninavyofikiri Kanisa lilivyo. Naam, nina Andiko kwa ajili ya jambo hilo, linalosema, "Msiogope, enyi Kundi dogo, ni mapenzi ya Baba yenu—yenu kuwapa ule Ufalme." Nami ningeninii...hilo ndilo Kundi dogo ninalotaka kuhesabiwa pamoja nalo kwenye siku ile, lile ambalo Yeye alisema, "Lisiogope." Nasi tuna furaha sana kwa ajili ya majaliwa ya kushuka kuja huku usiku wa leo.

2 Nami sikuja nikiwa na nia ya kuhubiri. Muda mfupi tu uliopita kulikuwako na mtu aliyekuja mlangoni, na wakati nilipokuwa katika kusoma, nikiandaa muktadha kwa ajili ya somo ninalotaka kutumia mara moja sasa katika mikutano ijayo ya Phoenix na Tucson, na kote kule. Nami nilikuwa nikilishwa chakula bora kweli katika Roho, mwajua, kwa mambo mazuri ya Mungu, kuhusu Mkataa, na lile somo juu ya *Mkataa*. Ndipo mke wangu akaja na akaniambia ya kwamba kulikuwa na mtu fulani aliyekuwa amekuja kuniona, nami si—sikusikia vizuri, ndipo baadaye, mbona, kasema, "Je! utakuwa huko chini kanisani usiku wa leo?"

3 Nami nikasema, "Nafikiri." Na nikaendelea kujaribu kudumu katika roho juu ya yale niliyokuwa nikifanya. Na akarudi na kusema ilikuwa ni mgonjwa aliyekuwa akija kuombewa. Nikasema, "Vema, basi, nitashuka niende kanisani, kwa vyovyote vile, unaona, na ni kuwaombea wagonjwa." Mimi daima, hiyo ni...Mnajua, mambo hayo ni...tunapaswa kuwaendea upesi iwezekanavyo wakati watu ni wagonjwa na wahitaji. Mtu yeyote ambaye amekuwa mgonjwa anajua jinsi ya kuthamini maana ya kuponywa na nguvu kuu za Mungu za uponyaji. Na ni jambo zuri sana, ni majaliwa ya jinsi gani.

4 Sasa, Jumapili ijayo, Bwana akipenda, Ndugu Neville na hao wengine wasipokuwa na jambo lolote maalumu, nilifikiri Jumapili ijayo asubuhi ni—ningewaletea watu ujumbe wangu wa Krismasi, kwa sababu kuwaacha—kuwaacha...Baadhi yao wanatoka mbali sana, wajua, na kama vile Georgia na sehemu mbalimbali, na hiyo itawaruhusu kurudi kwa wakati mzuri kununua vitu vya Krismasi madukani na kadhalika.

5 Na Billy ndiyo kwanza atoke aje na kuniambia, akasema dada yangu, Delores, Jumapili ijayo jioni kabla tu ya ibada, ana namna fulani ya zawadi ndo—ndogo kwa ajili ya watoto,

kipindi kidogo hapa wanachokiendea, mwajua, mchezo mdogo wa Krismasi wanaotaka kuufanya kabla ya ibada kuanza. Nami nikasema, “Vema, hiyo itakuwa Jumapili jioni sivyo?”

Kasema, “Naam.”

Nikasema, “Hilo halitakatiza kitu hata kidogo, basi.”

6 Sasa, mnaona, Jumanne ijayo ndio mkesha wa Krismasi, basi kama . . . ama Juma lijalo, jumanne, ni Krismasi. Kwa hiyo hilo lingewaharakisha watu, mnaona, halafu inawabidi kurudi nyumbani kwenye mkesha wa Krismasi, na Jumatatu, kwa hiyo nikawaza ya kwamba mimi . . . naam, majuma mawili. Hilo ni sawa, majuma mawili ni sawa. Kwa hiyo nikawazia labda ningekuja usiku wa leo na kuwajulisha watu, kama Bwana anapenda, na Ndugu Neville hana jambo lolote maalum. Ya kwamba, kwa kawaida mimi hupenda kuuleta ujumbe wangu wa Krismasi kwa kanisa, na ujumbe wangu wa Pasaka, na lolote Bwana analoweka moyoni mwangu kutoa. Na Jumapili ijayo, Bwana akipenda, Jumapili ijayo asubuhi nitatoa . . .

7 Na sababu ya mimi kuuchukua asubuhi badala ya jioni, ambapo watu wanaotoka mbali sana, wana alasiri ya kusafiri ili waweze kufika nyumbani, mnaona. Na ni afadhali ningeufanya usiku, nafikiri jioni ni bora zaidi. Ni—ninapenda ibada ya jioni, wakati jua linapotua, kitu, kitu kama hicho. Ilikuwa ni Mungu katika bustani ya Edeni, kwa Adamu, angekuja wakati wa jua kupunga na kuzungumza na Adamu. Mnaona, nami naipenda ibada ya jioni. Lakini, na jinsi hali ya mambo ilivyo hapa, kwamba ingekuwa ni bora kwamba niifanye asubuhi, basi ili kwamba watu wapate kuondoka.

8 Nami nina furaha ya kwamba maskani inaongezwa hapa nje kufikia mahali pengine huko kuzidi hapa tulipo, huku nafasi zaidi ikiongezewa. Baada ya wasiwasi mwingi na usumbufu, hatimaye tuliipata hata hivyo. Mwajua, maskini mzee Ndugu Bosworth alikuwa na ucheshi, alisema, “Mtoto mchanga anayelia kwa sauti kubwa zaidi ya wote ndiye anayeshughulikiwa zaidi.” Kwa hiyo kwa namna fulani hilo ni kama kusema mengi sana, mwajua, na kwa hiyo nafikiri ni vema kulia kidogo mara kwa mara, sivyo?

9 Kwa hiyo, basi nataka kumpongeza Ndugu Anthony na wenzake hapa kwa ajili ya muziki huo mzuri. Ndio kwanza niingie nikausikia huo. Na, mwajua, ala hizo ni tarumbeta. Nimetamani mmoja wa watoto wangu, angalau mmoja wao, acheze tarumbeta, mimi—mimi . . . na ala hizo za kupuliziwa.

10 Becky alianza kwenye piano, bali yuko kwenye kile kitu kidogo cha kitineja, mwajua, ambapo, anataka kuachana nayo sasa. Na—naye alianza . . . Mwalimu alisema ya kwamba itawabidi kuanza na muziki pendwa. Sio, sasa, simaanishi . . . mnajua ninalomaanisha, vianzio, na kadhalika, vya muziki dhati, kusudi wapate kuingiza muziki wa kidini kwake. Wakati

anapofikia kiwango cha juu cha huo, ndipo anawazia, “Vema, nitauacha tu.” Na mimi—mimi . . . watoto ni shida. Na, kwa vyovyote vile, haina budi iwe ni wito wa Mungu, kwa kuanzia. Ninaamini dada yake, Sara, huko nyuma atamshinda, hata hivyo, wala hajapata kufunzwa. Kwa hiyo, kwa hiyo basi wito wa Mungu ni bora wakati mtu una kipaji jinsi hiyo.

11 Lakini ninapenda tarumbeta. Ninakumbuka wakati walipoiweka wakfu maskani hii hapa nje pembeni, tarumbeta zilipigwa nusu siku hapa nje, “Pale msalabani ambapo Mwokozi wangu alifia, pale chini ambapo nilisihi nikilia nipate msamaha wa dhambi, hapo ndipo damu ilipakwa moyoni mwangu,” wakati nilipokuwa nikiingiza maandishi yangu katika jiwe la pembeni.

12 Nami ninakumbuka usiku mmoja katika kanisa la Utatu la Kimethodisti, wakati mzee Daktari Morrison . . . Wengi wenu enyi watu mlioishi huko nyuma katika siku zangu mnamkumbuka Daktari Morrison, mzee mtakatifu. Asbury ilipoteza mmoja wa watu mashuhuri sana tangu Asbury, walipompoteza Daktari Morrison, kwa umri wake, mzee mcha Mungu. Nami sikuzote nilipenda kumsikia akihubiri. Nami nilienda huko kumsikiliza kwenye kanisa la Utatu la Kimethodisti pale. Na usiku huo, wavulana wawili walitokea kwenye roshani ndogo wakati tu mimi na mke wangu tulipokuwa tukipanda juu, nao walikuwa wameinua tarumbeta zao hewani namna hiyo, na ala hizo hapo, nao wakauimba huo, “Pale msalabani ambapo Mwokozi wangu alifia!” Ule msalaba mkubwa pale juu, ukizunguka. Nilisimama tu mtaani na kuinua mikono yangu, nikaanza tu kumsifu Mungu mara moja. Nisingeweza kujizuia.

13 Kuna namna fulani ya mhemuko ndani ya Mkristo aliyezaliwa mara ya pili, wakati inapodunda, kuna jambo fulani halina budi kutukia, hakuna lingine. Loo, mimi . . . Hakuna kitu kama Mkristo wa mtindo wa kale. Hiyo ni kweli. Nisingelibadilisha na chochote, tukio langu, nisingelilibadilisha na utajiri wowote wa ulimwengu, ama ulimwengu wote, wala na mfumo wote wa jua na yote, kwa yale Yesu amenifundisha kumhusu Mwenyewe.

14 Kuna mtu fulani ambaye huketi nasi, kila wakati ninapotazama nyuma moyo wangu huruka. Ni mtu ninayemwona akila ushirika, hivi majuzi usiku, anatembea kwa mkongojo. Je! kuna mtu aliyepata kukwambia ya kwamba unafanana na Oral Roberts? [Huyo ndugu anasema, “Vema, ndugu, uliniambia, mara nilipoingia hapa sasa. Nimekuwa nikikungojea utambue jambo hilo.”—Mh.] Nawaambia, kila wakati mimi . . . Ni wangapi . . . Mmemwona Oral Roberts, karibu ninyi nyote. Kama yeye hafanani na Oral Roberts! Ilitokea tu niliangalia nyuma. Nami na—nafikiri yeye ni mkubwa kidogo kuliko Oral alivyo. Lakini kuangalia tu jinsi anavyozichana

nywele zake, na paji lake la uso na maumbo yake, na daima kwa namna fulani anaonekana ni mtu muungwana, anaketi kama Oral. Na kwa hiyo da—daima hufikiri, "Ndugu Oral?" Anaonekana tu kama yeye.

15 Ndugu Oral anaanzisha namna fulani ya shule ya Biblia huko mahali fulani sasa, ninaamini, ama kitu kama hicho. Nilisikia habari hizo hivi majuzi. Ni kitu gani? [Ndugu Neville anasema, "Chuo Kikuu."—Mh.] Chuo kikuu. Naam. Ndugu Carl Williams ni mmoja wa mkataa wake, kwa namna fulani, sijui ni kitu gani sasa.

16 Sasa, sasa kumbukeni, Jumapili, Bwana akipenda, tutaanza. Nina Pasaka...ama ujumbe wa Krismasi. Halafu nina—nina shukrani kuhusu kuanzishwa kwa maskani. Na basi natumai ya kwamba hii haitakuwa ni ongezeko tu la idadi, bali itakuwa ni nyongeza ya neema ambayo Mungu atalikirimia kanisa letu, huduma yetu, ninii yetu...sio huduma, bali kusanyiko letu ambao tumekusanyika pamoja. Tunalipenda.

17 Na—na ningetaka tu kusema jambo hili. Sitachukua muda mrefu. Lakini, nina mambo mengi ninayopaswa kusema, lakini sitayasema, ingechukua muda mwingi sana. Lakini, ningetaka kusema jambo hili, ni jambo ambalo siwezi kulisema. Kuna mambo (kila mtu anaelewa) ambayo unajua, na ni katika Jina la Bwana, hata hivyo huwezi kuyasema. Unaona, inakubidi kuyaweka moyoni mwako mwenyewe. Mnaona? Lakini tukio fulani ambalo linakaribia, na limekuwa likikaribia kwa muda fulani, ambalo liko karibu kutukia, ambapo nimeshangaa sana kumwona Roho Mtakatifu akitembea miongoni mwa watu kufikia mahali hapo, nao hawajui hata jambo moja la duniani, mnaona, bali kumwona Roho Mtakatifu akisogea kwenye hilo. Nitalifunua, Bwana akipenda, wakati fulani unaofaa. Sasa, kumbukeni, hiyo inaonyesha Mungu miongoni mwao.

18 Kama vile mtu fulani, ninaamini, ndugu, naam, alivyosema muda mfupi uliopita, Ndugu Neville alisema ya kwamba, "Mungu, hahesabu ku—kutokuwa na utaratibu kati yetu, kukosa kwetu adabu machoni Pake." Ya kwamba yule mwonaji aliyeenda kuwaangalia Israeli, na angeweza kuwaona kwa jicho lake la kawaida, na jinsi mambo yasivyokuwa na utaratibu, jinsi ambavyo walikuwa wametenda mabaya na wangepaswa kulaaniwa. Lakini kile askofu huyo alichoshindwa kuona kilikuwa ni ule Mwamba uliopigwa na ile Nyoka ya Shaba, mnaona, ikifanya upatanisho. Kwa hiyo, unaona, wakati—wakati Balaamu alipowatazama Israeli, aliona sababu ya kuwalaani. Unaona? Bali wakati Mungu alipowaangalia, Yeye aliona ule upatanisho. Akasema, "Wewe ni kama nyati." Amina. "Ni nani anayeweza kuweka chochote mapitoni mwako? U mcha Mungu jinsi gani, mahema yako ni yenye haki jinsi gani." Hivyo ndivyo Mungu alivyowaona. Mnaona? Si vile mwanadamu

alivyowaona, sio vile wa—watu wenye vyeo walivyowaona; bali jinsi Yeye alivyowaona.

19 Na, Ee Mungu, jalia hiyo iwe ndiyo sehemu yangu! Jalia hiyo iwe ni sehemu yangu, kwa kuwa sina kitu kwa nafsi yangu ninachoweza kudai. "Sina cha mkononi niletacho, ninaushikilia tu msalaba Wako." Unaona, huo tu ndio yote tuliyo nayo.

20 Vema, huu ni usiku wa mkutano wa maombi, ama si usiku wa mkutano wa maombi, bali hili hapa kwa namna fulani ni kundi la kiinjilisti. Sisi—sisi tunapenda kuliweka Neno. Na huenda ningetaka kuzungumza nanyi usiku wa leo kwa dakika chache. Wengi wenu ambao mngetaka kuyafungua Maandiko . . . Vema, je! hivi mnajua, jambo la ajabu, hicho kimefunguka mahali penyewe, kwenye fungu lenyewe nililotaka kusoma. Naam, bwana. Ajabu. Hilo lilikuwa ni Wakorintho wa Kwanza, mlango wa 11, na mihtasari niliyokuwa nimeandika hapa chini, mahali fulani hapa ndani, ambayo nilikuwa nikiwazia, kama naweza kupapata sasa, katika Wakorintho wa Kwanza m—m—mlango wa 11. Hii hapa, papa hapa. Naam, bwana.

21 Sasa, kabla hatujaliendea Neno, hebu na tumwendee Mwandishi, mnaona, Ambaye ni Neno, tupate kuomba rehema na baraka Zake tunapomsoma Yeye ambaye ni Neno. Na tuombe.

22 Ee Bwana Mungu, uliyejaa neema na rehema, ambaye umekuwa radhi kote katika wakati, baada ya mwanadamu kutenda dhambi na kuweka lile shimo kubwa kati yake na Wewe, shimo ambalo asingeweza kujivusha kurudi mwenyewe. Yeye alikuwa amepotea kabisa, kabisa, pasipo na njia ya kurudi. Lakini Mungu wa . . . aliyejaa neema yote, alikuwa tayari kuchukua Kibadala mahali pake, ndipo akamrudisha. Hilo limeisisimua mioyo ya wote waliopata kukujua Wewe, Bwana, jinsi ambavyo katika upendo na neema Yako kuu Wewe ulichukua Kibadala! Na kama vile ndio kwanza tumalize kulielezea, Bwana, tunakitegemea Kibadala hicho usiku wa leo, Yule aliyekufa badala yetu sisi wenye dhambi, Yule Mwenye Haki ambaye alichukua juu ya nafsi Yake dhambi zetu. Tunamtumaini Yeye.

23 Sasa kwa uchaji tunakuja kwenye Neno Lake, tukiwa na mioyo na vichwa vilivyoinamishwa, katika uchaji na katika heshima na katika shukrani. Na tukiomba ya kwamba Wewe utatutumia usiku wa leo, neema, kwa Roho Mtakatifu, na utatupa M—Mkate wa Uzima tunaohitaji kutudumisha. Unajua kile hasa tunachohitaji, nasi tunajua ya kwamba Wewe umeahidi ya kwamba kama tukiomba tutapokea.

24 Tungekumbuka usiku wa leo, Bwana, wale wote tunaojua ni wagonjwa na wahitaji, kwamba watapewa neema ya Mungu kwa wingi mno. Na, Baba, tunawaombea wale walioanguka, ya kwamba sikukuu hii ijayo italeta kumbukumbu moyoni

mwao, ya kwamba kutoka mahali walipokuwa wakati mmoja, na wameanguka kwenye sehemu ya nje ya ushirika Wako. Mungu, tunaomba ya kwamba watarudi (tujalie, Bwana), warudi kwenye kusanyiko, kwenye—kwenye Kusanyiko la Mzaliwa wa Kwanza, warudi mahali palipo na neema na rehema, na upendo na wema, na uponyaji wa nafsi zetu, nia zetu na miili yetu. Tujalie, Bwana. Libariki Neno usiku wa leo. Tuimarishe sisi sote, na utupe Baraka Zako, tunapoomba katika Jina la Yesu. Amina.

25 Sasa, kwa dakika chache tu ningetaka kuvutia usikivu wenu kwenye Wakorintho wa Kwanza, mlango wa 11, kifungu cha 23, 24, na 25.

> *Kwa maana mimi nalipokea kwa Bwana niliyowapa ninyi, ya kuwa Bwana Yesu usiku ule aliotolewa alitwaa mkate,*
>
> *Naye akiisha kushukuru akaumega, akasema, Twaeni, mle: huu ndio mwili wangu uliovunjwa kwa ajili yenu; fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu.*
>
> *Na vivi hivi baada ya kula akakitwaa kikombe, akisema, Kikombe hiki ni agano jipya katika damu yangu, fanyeni hivi kila mnywapo, kwa ukumbusho wangu.*

26 Kama ningeweza kuliita hili fungu dogo tu la maneno ambalo ningetaka kulirejea, lingekuwa ni hili: *Kumkumbuka Bwana*. Linasikika kama usiku ambao. . . ama ujumbe ambao ulipaswa kuhubiriwa Jumapili iliyopita, kwenye meza ya Bwana. Lakini nataka kuliendea katika mwelekeo tofauti kidogo tu kwa dakika chache, tunapokusanya mawazo ye—yetu pamoja, na katika kumwabudu Bwana.

27 Tungeweza, hakika, kuanzia na meza ya Bwana, kwa sababu hapo ni mahali pazuri ambapo sisi sote tunapakumbuka. Kumkumbuka Bwana kwenye meza Yake, ambapo, kwa kweli, fungu hili la maneno linarejea kwenye hilo. Lakini, hilo ni kusema, Paulo alisema ya kwamba inatupasa kukinywea kikombe hicho na—na kuinywa da—damu, na kula ule mkate wa kosha, kwa ukumbusho, kukumbuka yale aliyotufanyia. Na m—mnapofanya hivyo, hamtaki kulifanya ni jambo tu la kawaida, la kila siku; mnataka kweli kuja, mkimkumbuka Bwana. Mnaona? Kumbuka ya kwamba ilikuwa ni neema Yake na rehema Yake, na hiyo peke yake, inayokupa tumaini la pekee ulilo nalo. Haidhuru ungewahi kufanya nini, hakuna kitu popote ambacho kinaweza kwa vyovyote kukaribia kile Kristo alichokufanyia.

28 Nimekuwa na tukio la kuhuzunisha juma hili, na hata hivyo ni lenye utukufu sana, ningeliliita, nilimzika ndugu ambaye wakati mmoja aliketi pamoja nasi hapa. Na wengi wenu mnaujua wakati huo. Ilikuwa ni Ndugu yetu Rogers mwenye fadhili, Busty Rogers, kama tulivyomwita, Everett. Na

Ndugu Banks Wood hapa, na Ndugu Sothmann, tulienda pamoja kwenye ibada ya mazishi.

29 Na—nami niliendeshwa kwenye theluji, mpaka mahali pale pa kale nilipomzika kwanza, kama miaka ishirini na mitano iliyopita. Wakati huo nilipomzika, ilikuwa ni kwenye maji ya matope, katika Jina la Bwana Yesu Kristo. Tulipopitia kwenye lile daraja linalojulikana la Kivuko cha Maji Mafupi cha Totten, nilikuwa nikizungumza na ndugu zangu, na kusema, "Siku moja wakati mhudumu fulani wa kimadhehebu alipokuwa na hema ku—kubwa pale, yeye alisema, 'Maskini mlokole yule mdogo kule chini kwenye lile kanisa la Kibaptisti, ambaye anawabatiza watu katika Jina la Yesu Kristo,' akasema, 'kama mtu yeyote ambaye alipata kubatizwa jinsi hiyo, hata asingekaribishwa chini ya hema langu.'"

30 Na kwenye wakati huo ilitokea kwamba walikuwapo baadhi ya watu wameketi pale waliokuwa wamebatizwa katika Jina la Bwana Yesu, na huyo alikuwa ni Ndugu George Wright na familia yake. Walininii tu . . . Jambo pekee wangaliweza kufanya ni kutorudi.

31 Kwa hiyo siku ile kwenye kivuko hicho cha maji mafupi, loo, yeye kwa namna fulani aliuacha kabisa mkutano wake na alikuwa ameshuka kuja kutuangalia, nalo kusanyiko lake lilikuwa limesimama pale. Nami nikaenda mahali pale. Na kulikuwa kumenyesha mvua pale kilimani, nayo mashamba ya matope yalikuwa yameingiza matope, vijito vyake vidogo vilikuwa vimeufanya ule Mto wa Blue kujaa matope. Niliingia majini, kina cha kufikia kiunoni. Nami . . . Mmoja wa wadhamini, ama mashemasi, hasa, akanipa Biblia, nami nikasoma mahali ambapo Petro alisema kwenye Siku ya Pentekoste, "Tubuni, kila mmoja wenu, na mbatizwe katika Jina Lake Yesu Kristo mpate ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu."

32 Ilikuwa ni ile siku ambayo Georgie Carter alikuwa amelala pale, akijaribu kuinua mikono yake, akiwa na uzito wa ratili sitini na kitu tu, alikuwa amelazwa kitandani muda wa miaka tisa na miezi minane, bila kusogea. Nao watu wake, kanisa alilokuwa mfuasi wake, lilikuwa limesema, kama mtu yeyote hata akija kwenye mkutano wangu, wangefukuzwa kutoka kwenye ushirika wao kanisani. Na kwa hiyo ilikuwa ni jioni iyo hiyo ambapo aliponywa mara moja. Halafu alitaka kubatizwa kama msichana mdogo wa Nail aliyekuwa sehemu za huko juu; ambaye nilikuwa nimeona ono, nanyi mnajua hadithi hiyo, mikono yake na miguu imekunjamana; nami nikaenda katika ono na nguvu za Roho, nikamwekea mikono, hapo akatoka na akaponywa. Na kwa hiyo alikuwa mfuasi wa lilo hilo. Vema, lilikuwa ni kanisa la Methodisti. Huyo mhudumu wa Kimethodisti, Ndugu Smith, ndiye aliyekuwa amesimama ufukoni pamoja na kusanyiko lake.

33 Basi nikaanza kubatiza katika Biblia, ubatizo wa Kikristo. Na yapata wakati huo nilipokuwa nimewabatiza watu watano ama sita, mara ile mistari na foleni zikavunjika, huko kilimani. Hili hapa kundi hilo la Methodisti linashuka moja kwa moja wakiwa wamevaa nguo zao nadhifu, wapate kubatizwa katika Jina la Bwana Yesu. Na mmoja baada ya mwingine, akina mama wakiwa na nguo zao nzuri za hariri na mavazi ya kiangazi, wakipitia kwenye matope hayo, wakipangusa nyuso zao kwa machozi, huku rangi ya midomo ikisafishwa, wakija ku—ku—kukiri na—na kubatizwa.

34 Na pamoja na kundi hilo, mtu mmoja mwenye nguvu, mabega mapana, kitu kama mtindo wa nywele wa GI, uso mpana, mtu aliyeonekana mshupavu alienda pale, amevaa suti yake nzuri ya sufu ya bluu. Akasema, "Mimi, pia, nimejiamulia." Huyo alikuwa ni Busty Rogers, bila mtu yeyote kumwambia chochote. Hapo nikamzika katika Jina la Bwana Yesu Kristo, juu ya maungamo yake.

35 Na juma lililopita nilimweka kaburini huko Milltown. Nami nikahubiri somo la: *Ukamilifu Wa Ufufuo*. Nimekuwa Mmishenari, na kuona miungu mbalimbali na wanafalsafa; na hivyo ndivyo kila moja wa hizo ilivyo, nje ya Ukristo, ni falsafa tu, jinsi ambavyo wanaamini *hili, lile*, ama *linginelo*. Lakini yule Muumba mkuu aliyeumba viumbe! Hapana budi kuwepo na Muumba kama kuna uumbaji. Na kama kuna uumbaji, ulifanywa na Muumba. Na kazi ya mtu yeyote humwakisi mwenyewe. Yeye ni seremala mzuri, anafanya kazi nzuri, anajenga. Na endapo ni makanika mzuri, anafanya kazi nzuri. Kazi yako hukuakisi tu. Nao uumbaji wa Mungu humwakisi Mungu. Na Mungu aliumba kila kitu kwa kusudi fulani. Na kila kitu kinachotumikia kusudi la Mungu, wakati kinapokufa, kina ufufuo. Niambie kitu kimoja. Nami nilileta vitu vingi, kama maua na miti.

36 Na jinsi ambavyo jua huchomoza asubuhi, mtoto mchanga aliyezaliwa, ni mnyonge, miali yake. Karibu saa nne, ni tineja. Na saa sita linawaka katika nguvu zake, katika uzuri wa uanamama ama uanaume. Na karibu saa nane alasiri, linakuwa karibu kama mimi. Na halafu kufikia saa kumi na moja alasiri, linakuwa kama babu, linalala chini. Na hatimaye miali yake inapoa ardhini, na linakufa. Je! huo ndio mwisho wake? Lilitumikia kusudi la Mungu. Lilikuza uhai wa mimea lilipokuwa likipitia ardhini. Mimea ambayo ingalikufa mwaka jana, liliifufua. Je! huo ndio mwisho wake wakati linapotumikia kusudi la Mungu? Linafufuka tena kesho yake asubuhi, na maisha mapya! Kila mti unafanya vile vile, chochote kile, kila kitu, mwezi, nyota, mfumo wa jua na sayari zake, kila kitu kinaahidi.

37 Na kama mtu anatumikia kusudi la Mungu, kuna ufufuo hakika kama chochote kile. Jambo pekee linalopaswa kufanya, ni, Mungu anangojea tu wakati, kama vile anavyofanya sasa.

38 Majani makubwa ndiyo kwanza yaanguke kutoka mitini, yameanguka, hasa. Ambapo mekundu, kijanikibichi, bluu, hudhurungi, rangi zote mbalimbali kote kwenye mapana ya nchi, ambapo viumbe vya Mungu vilikuwa chini yake vimekufa, Mungu alipanda tu shada lake la maua. Lakini Yeye anajua wakati anapopanda shada la maua, kuna ufufuo katika msimu wa kuchipua! Ulimwengu hauna budi kuja tu huku katika mzingo wake mpaka unaporudi moja kwa moja ukawa sawa na jua tena, nao utafufuka katika maua ya mazishi.

39 Kamwe usiseme, "Huu ndio mwisho," si zaidi ya vile majani, yaliyo na rangi ya hudhurungi mtini, yanavyosema huo ndio mwisho. Jambo pekee linalopaswa kufanya, ni duara la majira ya Mungu kuelea huku na huko, mpaka kwenye wakati wa kuja kwa Mwana wa Mungu. Na kila kiumbe kilicho hai kilichopata kufa katika Kristo kitafufuka tena. Katika Uwepo Wake, kumkumbuka Yeye. Loo, nitakapofikia mwisho wa safari yangu, ninataka kufa katika Uwepo Wake, nikimkumbuka, ya kwamba Yeye Ndiye ufufuo na Uzima. Yeye Ndiye Huo.

40 Basi tunapokuja kwenye meza ya Bwana. Meza ya Bwana, kama nilivyoielezea hapa hapo kabla, siyo. . .Tunaamini kile tunachokiita "ushirika" ni—ni kuula mkate. Tunaweka kitu ki—ki—kibaya. . .Tunaweka kitu sahihi mahali pabaya. Mkate sio unaojalisha, divai siyo inayojalisha, huo ni mkate wa kosha na divai. Lakini jambo ambalo, ni, *ushirika* maana yake ni "kuzungumza na," na, katika kuzungumza na Yeye, kumkumbuka. Nafikiri ndio wakati uliobarikiwa sana wa ibada. Mnaona? Kila saa ya maisha yetu inapaswa kuwa ni ushirika.

41 Ushirika na Bwana ni kama oasisi jangwani. Ni kama chemchemi chini ya kidimbwi, mahali ambapo m—msafiri akipita, anasimama na kuyanywa maji mpaka anakata kiu yake. Hiyo ni kumkumbuka Bwana. Kuja kwa utaratibu wa meza Yake, ambapo msafiri apitaye ambaye—ambaye ni mgeni pamoja nasi hapa duniani, pamoja, kwamba tunaweza kuja mezani Pake, na hapo tuzinywee Baraka Zake na neema Yake na Neno Lake, katika ushirika kwenye Neno Lake, mpaka nafsi zetu zenye kiu ziridhike. Na kisha tunaondoka mahali hapa pa kuabudia, tumeburudika, tumeridhika; tukitoka kwenda kukabiliana na shida za jangwani tena, shida za maisha ya jangwani. Naam, oasisi jangwani, tukijiburudisha, tukijifariji wakati tunapoona kiu.

42 Inapaswa kuwa na kila mwaminio. Inaridhi-. . .Ndivyo ilivyo na kila mwabuduo wa kweli, ya kwamba wana shauku ya kukutana pamoja. Kuna jambo fulani kuhusu ushirika ambalo—ambalo ni la Kiungu, limeamriwa na Mungu, na ni takakatifu, safi. Nao wenye haki wanalionea kiu.

43 Kama vile Daudi alivyosema, ya kwamba "nafsi yake ilimwonea Mungu kiu, kama ayala alivyoionea mito ya maji."

Maskini kulungu aliyejeruhiwa ambaye mbwa mwitu walikuwa wameng'wafua kipande cha nyama kutoka ubavuni mwake, na ki—kimeng'wafuliwa kutoka kwake. Naye amesimama, akihema na kuhadhari. Ambapo, akinusa kwa hisia aliyopewa na Mungu, anaweza kunusa harufu ya maji kwa maili kadhaa. Naye anakishikilia maskini kichwa chake hewani huku uhai wake ukiendelea kutoka kwa kutokwa na damu. Naye anajua, kama kamwe anaweza kuifikia ile chemchemi, ya kwamba anaweza kuishi. Hakuna mtu atakayemshika basi. Akiwahi kuyafikia maji, atampumbaza kila mbwa ungaliweza kumfukuza nao, kwa maana anajua a—amepata tegemeo la uhai.

44 Na wakati kanisa linapofikia mahali hapo, ambapo kwamba Kristo ni muhimu sana kwetu hata tunaona kiu kufika kwenye Uwepo Wake na sisi kwa sisi, ni Tegemeo litoalo Uzima. Hakuna ibilisi anayeweza kukushinda. Hata mauti yenyewe imeshindwa hapo. Loo, ni tumaini la jinsi gani! Ni mahali pa jinsi gani! Kujiburudisha wenyewe. Na, katika kufanya jambo hilo, tukikumbuka Kristo Ndiye aliyefanya hilo liwezekane kwetu. Yeye Ndiye aliyetufanyia mambo haya, hatuna budi kumkumbuka. Kwa kuwa, kumbukeni, wakati mmoja tulikuwa wageni na bila Mungu, Wamataifa, tumechukuliwa na sanamu bubu. Lakini, kumbukeni, Kristo alikufa si kwa ajili ya Myahudi, bali kwa kila kiumbe cha jamii iliyoanguka ya Adamu, Kristo alikufa.

45 Tunapokuja kumkumbuka kwenye chemchemi yake ya—ya ushirika, i—inapaswa kutukumbusha huko nyuma wakati kama vile Israeli walipokuwa katika safari yao. Nao wakaja, hata hivyo kwenye wajibu wao hasa, wakiwa njiani kutoka Misri kuelekea kwenye ukombozi wao, kwenye nchi ya ahadi, na, katika kutekeleza wajibu wao, waliishiwa na maji. Na kila mahali palikauka palivyoonekana, sehemu, kila . . . chini ya kila kilima ambapo panapaswa kuwa na chemchemi ya maji, hakukuwako na yoyote. Nao walikuwa wakiangamia jangwani. Ndipo ukatokea ule Mwamba, ambapo Musa aliupiga Mwamba huu na kutoka kwake yakafoka maji tele. Kila mtu aliyekuwa na kiu, kila mwanamke aliyekuwa na kiu, mtoto, ama hata kila mnyama aliyekuwa na kiu, angeweza kunywa maji kwa wingi.

46 Kama vile Yohama 3:16, lile fungu la thamani sana la Biblia, lilisema, "Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili kila aaminiye (anayeamini, anayeshiriki, anayemkumbuka Yeye) hataangamia, bali atakuwa na Uzima wa Milele." Tukikumbuka Kristo alikuwa Ndiye Mwamba wetu uliopigwa, apate kuuokoa ulimwengu unaoangamia, Mmataifa anayeangamia, Myahudi anayeangamia, ulimwengu unaoangamia. Kristo aliutoa uhai Wake kwa wingi, kusudi kila mtu aliyeona njaa na kiu, alisema nabii, "Haya, njoni kwenye chemchemi, nunueni kutoka Kwangu

maziwa na asali bila thamani." Njoni, kwa kuwa ni ushirika, njoni katika ukumbusho wa Bwana.

47 Ninaweza kuwazia juu ya kumkumbuka Bwana tena kwenye mahali pa faraja, katika kile kisima kilichoitwa *Beerlahairoi*, ambalo linamaanisha katika lugha ya Kiebrania, "Kisima cha Yeye aishiye na anayeniona." Hajiri, alieleweka vibaya, hata hivyo akiwa kwenye wajibu wake. Alieleweka vibaya, akalaumiwa, na akafukuzwa, bila mahali pa kwenda, pamoja na mtoto aliyekuwa akifa, nayo maji yalikuwa yamekwisha kwenye chupa. Na maskini jamaa huyo alikuwa akilia. Na ni moyo wa mama tu ungaliweza kujua maana ya kusikia kilio hicho cha maji, huku maskini ulimi wake mdogo ukivimba, na midomo yake imekauka sana, na mtoto wake akidhoofika kila dakika. Amefukuzwa, moja kwa moja kwenye wajibu, hana mahali pa kwenda. Mwenyewe, alikuwa amekaa bila yoyote, hata akaminya tone la mwisho juu ya midomo yake iliyokauka sana. Na kisha ile chupa ikakauka, naye akaiweka chini na kuondoka. Naye maskini jamaa huyo mdogo akililia maji, na alizidi kudhoofika na kudhoofika; na ni mtoto wake wa pekee.

48 Hapana shaka ila moyo wake usio na hatia ungelia, "Ee Mungu, nimefanya nini? Nimefanya nini?" Na asingevumilia kumwona mtoto huyo akifa mikononi mwake, kwa hiyo akamlaza chini ya kichaka. Naye akaenda kama mwendo wa kutupwa kwa mshale, labda yadi mia moja au zaidi, naye akaona mti mdogo, ndipo akapiga magoti na hapo akaanza kulia. Kwa maana alishangaa, "Kwa nini?" Kama alifanya yaliyo sawa, mbona jambo hili limjie? Mara nyingi tunawazia hivyo juu ya magonjwa yetu na mateso, mnaona, bali labda yote yanafanyika kuonyesha neema na rehema. Na wakati alipowazia, alisikia maskini vilio vidhaifu wakati hatimaye vikififia kabisa, kwa ajili ya maji.

49 Akasikia Sauti ikinena na kusema, "Kwa nini unalia? Unalilia nini?"

50 Ndipo akaangalia juu, na akaona kisima kikibubujika. Ni chemchemi ya faraja jinsi gani! Beerlahairoi, huenda nikalitamka hilo vibaya. B, e maradufu, r-l-a-h-a-i-r-o-i, ambalo maana yake ni, "Kisima cha Yeye aliye hai na anayeniona! Yeye asiyeweza kufa! Melkizedeki! El Shaddai! Yeye aishiye na anayeniona, akijua haja zangu, amenikumbuka. Na hapo akanikumbuka kama nilivyomkumbuka, nami ninajua ya kwamba Yeye yu hai na amebubujika hapa jangwani, kisima hiki."

51 Loo, hivi tunaweza kutumia hilo katika ujumbe wa saa moja sasa hivi, juu ya siku hizi sasa, wakati jangwa la makanisa, madhehebu, na—na i—i—injili ya wahubiri wa jamii na mi—mitindo ya ulimwengu imenyemelea ikaingia ndani, na imeunda madhehebu na kuvunjika.

52 Na halafu kuwazia ya kwamba hapo panasimama tena usiku wa leo, kisima cha yeye aishiye na ananiona mimi. Hivyo ndivyo kumkumbuka Kristo kunapaswa kumaanisha kwa mwabuduo. Naam. Loo, yeye alieleweka vibaya na akatupwa nje. Yesu alisema, wakati alipokuwa hapa duniani, "Mimi Ndimi Maji yaliyo hai, Mimi Ndimi Maji ya Uzima."

53 Nami ninataka kuchukua wazo lingine dogo hapa linalokuja niani mwangu. Wakati Yesu alipokuwa hukumuni, na si kwa kitu kingine ila kwa ajili ya dhihaka, na . . . Yeye alipelekwa kutoka kwa Pilato mpaka kwa Herode. Sasa, haikumbidi Pilato kufanya hivyo, na, mwajua, hata alijaribu kuiosha mikono yake ajiondolee hilo. Lakini akiisha kuwa mikononi mwako, huna budi kujiamulia. Huwezi kulisukumia kwa mtu mwingine. Ni wewe, kama mtu binafsi. Lakini Yeye, Yeye alipelekwa kwa Herode, ku—kumfanyia tu dhi—dhihaka, kwa sababu Yeye alikuwa na jina mashuhuri la kuwa mfanya mwujiza na kadhalika, na alikuwa aliyetupwa nje kutoka kanisani. Kwa hiyo Pilato mwenyewe, alifikiri angempeleka tu kwa Herode, na huenda hilo lingetatua ile chuki ya kale waliyokuwa nayo, mmoja kwa mwingine.

54 Na kwa hiyo Yesu alivushwa mitaani na kushushwa kwenye sehemu nyingi mpaka akakutana na mahakama kuu, Herode. Na alipokutana na Herode, naye Herode akapewa nafasi yake ya pekee! Mtu anaweza kuwa mjinga kiasi gani? Laiti Herode angalijua ya kwamba hapo mbele yake likisimama lilikuwa ni timizo la kila nabii wa Kiebrania, la shauku, kiu ya ulimwengu, ambalo lilisimama mbele yake, timizo la kila mtu mwenye hekima na nabii aliyepata kunena. Nafasi ya kuuridhisha moyo wake wenye dhambi kwa neema na rehema. Alikuwa ni mtu mjinga jinsi gani!

55 Na hata hivyo si mjinga kiasi kama cha mtu leo hii ambaye anakabiliwa na kitu kile kile kwa maana tumekuwa na muda wa miaka elfu mbili zaidi wa mafundisho Yake, wa rehema Yake. Lakini ni jambo la ki—kijinga jinsi gani ambalo Herode alifanya wakati aliposimama mbele Yake wala kamwe hakumwomba neema na rehema, kamwe hakuomba msamaha wa dhambi. Kamwe hakujua ya kwamba akisimama . . . sidhani mtu huyo alitambua ya kwamba hapo akisimama mbele zake alikuwa ni Mtu kama huyo. Hebu na tuliache hilo lizame kwa dakika moja. Kwa sababu mtu huyo hakuwa na ji—jina kubwa sana katika jamii, kwa mashirika mbalimbali na—na vilabu, na kadhalika, ambavyo alihusishwa navyo. Hakuwa na jina kama hilo.

56 Bali alikuwa nalo, miongoni mwa watu walioijua Biblia na kujua ahadi. Na hebu nilitilie mkazo zaidi, hao waliochaguliwa tangu zamani kwa Uzima wa Milele, walitambua jambo hilo mara aliposimama pale.

57 Lakini Herode hakuwa amejifunza jambo hili, hakulijua. Ni jambo la kuhuzunisha jinsi gani. Yote ambayo manabii walikuwa wamenena habari zake kwa muda wa miaka elfu nne, timizo la kilio cha ulimwengu lilisimama mbele yake. Hapo mbele yake ulisimama utimilifu wote. Na kama vile ningeweza kusema jambo hili tena, tungewazia yeye alikuwa ni mtu mjinga maana alifanya uamuzi wa kijinga, kwa kuwa, mnaona yeye kamwe hakumwomba rehema. Alimwomba a—amburudishe. "Loo, nimesikia ya kwamba Wewe ni m—mfanya mwujiza." Aliomba burudani badala ya rehema.

58 Hivyo ndivyo ulimwengu, leo hii, unavyotoa tena ule uamuzi wa Herode, wakati wanapomwona Kristo mfanya-miujiza akifanya jambo lile lile leo hii alilofanya wakati huo, na mambo pekee wanayohitaji, "Hebu nikuone ukifanya *hivi* na *vile*." Ati mnasema Herode atakuwa na mahali pabaya pa kusimama? Mtu wa siku hizi atakuwa na mahali pabaya zaidi pa kusimama! Herode alikuwa na ujuzi wa miaka elfu nne, manabii na watu wenye hekima. Tuna miaka elfu sita, pamoja na mafundisho mazuri mno ukilinganisha na waliyokuwa nayo siku hizo. Hakika. Ni jambo la jinsi gani lililofanya! Ndivyo ilivyo siku hizi, jambo lile lile!

59 Shida ilikuwa ni nini? Herode kamwe hakulitilia maanani sana. Hakutulia aliwazie hata kidogo.

60 Na hivyo ndivyo ilivyo na watu wa siku hizi. Wanaliona jambo hili kuu, limewashangaza sana, bali hawatulii muda mrefu vya kutosha. Wanajaribu kumsikiliza rabi fulani ama mwanatheolojia fulani anayelielezea vinginevyo kabisa. Na hata hivyo, jinsi ambavyo ninapowazia juu ya Jeffersonville, ni mara ngapi ningewafunika kama vile kuku angevifunika vifaranga wake, wala hamkutaka. Ni mara ngapi ningaliwakusanya? Ni mara ngapi ningeliufanya huu sha—shamba la kielelezo ambamo mataifa yote wangeruka waje huku, wala hamkutaka. Mnaona? Mnaona?

61 Sasa, mnaona kile kitakachombidi Herode kukumbuka katika siku ile? Nafasi yake nzuri sana, aliikataa. Na huko ng'ambo mahali fulani katika yale maeneo ya waliopotea, usiku wa leo, yeye anakumbuka yale aliyofanya kuhusu jambo hilo. Hilo limechelewa sana sasa.

62 Msiache jambo hilo liwe kwetu. Huu ndio wakati wetu wa kuzuriwa. Hebu na tumkumbuke Kristo, kwamba ni yeye yule jana, leo, na hata milele, Waebrania 13:8. Usingojee mpaka maeneo fulani huko, katika waliolaaniwa, katika kile kiwango usichoweza kuingia katika Uwepo wa Mungu, na wakati wako umekwisha duniani, katika jinamizi za kutisha utakumbuka ulikuwa na nafasi yako nawe ukaipuuza. Hebu vijana waliangalie jambo hili. Hebu wote na waliangalie.

63 Herode hakuliwazia kwa uzito sana. Nafasi yake ya pekee, yeye aliomba tu aburudishwe, na kwamba Yesu angefanya namna fulani ya kitimbi, atoe sungura kutoka kwenye kofia, ama, mwajua, ama jambo fulani. Aliwazia huenda akawa, kwa maneno mengine, alimfikiria kama mchawi. "Tumesikia ya kwamba unaweza kufanya mazingaombwe. Hebu nikuone ukifanya mazingaombwe Yako sasa."

64 Na hebu niseme jambo hili kwa uchaji. Lakini ni mara ngapi wale wanaojiita wahudumu wa siku hizi, wamesema, "Kama kukiwako na Roho Matakatifu, kama unaamini ya kwamba Roho Mtakatifu ni kama tu alivyokuwa hapo mwanzo, hebu nikuone ukimchukua maskini *Nanii* hapa, ama *huyu*, loo, mtu *huyu* hapa, mwanamke *huyu* hapa. Nitaenda niwalete. Hebu nikuone ukifanya hivyo."

65 Je! wanatambua ya kwamba huyo ni roho yule yule (la, hawatambui) aliyemwambia Yesu, "Kama wewe ni Mwana wa Mungu, chukua, yafanye mawe haya mkate. Kama Wewe ni Mwana wa Mungu, twambie ni nani aliyekupiga kichwani. Kama Wewe ni Nabii, twambie ni nani aliyekupiga," akiwa amefungwa kitambaa usoni Mwake. Wakampiga kichwani, kisha wakapitishiana kijiti hicho mmoja kwa mwingine, wakasema, "Twambie, kama Wewe ni Nabii. Twambie ni Nani aliyekupiga, tutakuamini basi. Twambie, kama Wewe ni Mwana wa Mungu. Sisi ni waaminifu mioyoni mwetu. Kama Wewe ni Mwana wa Mungu, shuka mtini nasi tutaamini Wewe ni Mwana wa Mungu."

66 Sijui kama watu wengi siku hizi, wote wanaume, wanawake, vijana kwa wazee, hawasimami mahali pale pale. Nawe utakumbuka, siku moja, ya kwamba ulikuwa katika Uwepo Wake, kwenye Chemchemi Yake; nawe ulitaka kuona kitimbi, ama ulitaka kuona mazingaombwe ama chochote kile kingine, "Hilo lingenifanya niliamini. Hebu nihisi mtetemo mgongoni mwangu, na hebu nifanye *hili* ama *lile*, nitaliamini." Mnaona, mhemuko fulani, ni ibada dhahiri ya sanamu! Hebu ni-. . .

67 Mnajua, Yesu alisema katika kisa kimoja, aliuliza swali. Ningetaka kuliuliza kanisa usiku wa leo jambo hili. Yesu alisema, "Kwa nini? Kwa nini? Kwa nini mnaniita 'Bwana' wenu, wala hamfanyi mambo niliyowaamuru mfanye? Mngewezaje kuniita 'Bwana,' wala hamlishiki Neno Langu? Kwa nini kuniita 'Bwana," na huku mnayakana mambo ambayo nimewaamuru kuhubiri na kufundisha?" Ni kitu gani? Ni kitu gani kinachofanya jambo hilo? Ni kwa sababu mapokeo fulani ya kimadhehebu yanasimama kati yao na Neno. Na kitu chochote kinachosimama kati yako na Mungu, ni sanamu, kinapachukua mahali pa Mungu. Kwa nini kukuita "Bwana"? *Bwana* maana yake ni "umilikaji," Bwana anamiliki mali. Na kama Mungu ananimiliki, kama mimi ni Wake, na Yeye alinigeuza siku moja wakati nilipokuwa kwenye njia mbaya, na akaniita kwa kusudi

fulani, napaswa kufanya nini ila kutimiza mapenzi Yake, kama Yeye alivyomfanyia Paulo. Ninawezaje kufanya jambo lingine lolote mbali na kulitimiza Neno Lake? "Kwa nini mnaniita 'Bwana'?"

68 Ninataka kumwita jamaa mwingine hapa, tuone kumhusu. Vipi kumhusu Yuda, kile anachopaswa kumkumbuka nacho? Tunazungumza juu ya kumkumbuka Bwana. Yuda usiku wa leo na, loo, hata wakati hatakuwapo tena, hana budi kukumbuka ya kwamba yeye aliuza haki zake za mzaliwa wa kwanza. Alimuuza Yesu apate faida ya kibinafsi. Tunamdhihaki Yuda. Tunasema alikuwa ni jamaa mbaya, mchafu, hastahili mahali popote ama jamii yoyote, hastahili kwenda Mbinguni. Kwa nini? Yeye alimuuza Bwana wake, baada ya yeye kuwa na nafasi hata ya kuwa mwa—mwanafunzi, kuwa mtume, wito ulio wa juu zaidi katika Biblia, wa juu kuliko nabii. Alikuwa na nafasi kuwa m—mtume, na akaiuza haki hiyo kwa ajili ya faida ya kibinafsi. Na sasa hana budi kukumbuka jambo hilo. Hivyo ndivyo anayomkumbuka Yesu: faida ya kibinafsi.

69 Nami sijui ni wangapi wao usiku wa leo bado wanasimama mimbarani, wangali wanavaa joho la kwaya, wanaketi kwenye kiti cha shemasi, ama wanachukua mahali pa mweka hazina, mdhamini, ama chochote kile, nafasi yake kanisani, ama mhudumu mimbarani, na wangali wanauza nafasi yao kwa ajili ya sifa ya kibinafsi, "Daktari, Askofu *Nanii*," kwa ajili ya sifa ya kibinafsi, faida ya kibinafsi.

70 Mtu fulani aliniambia wakati mmoja, "Ninaamini hiyo ni Kweli. Lakini kama ningehubiri jambo hilo, ningekuwa nikiomba-omba mtaani."

71 Je! mnamkumbuka yule tajiri na Lazaro, mahali pao pa mwisho na pa Milele palipokuwa? Ingawa mmoja alikuwa na . . . alikuwa ni ombaomba, na huyo mwingine alikuwa ni tajiri, lakini picha ilibadilika siku moja na wote wawili waliweza kukumbuka. Kwa hiyo, watu wanapiga makelele usiku wa leo kuhusu Yuda aliyemuuza kwa ajili ya faida ya kibinafsi, na wengi sana wanafanya jambo lile lile siku hizi, wanamuuza kwa ajili ya faida ya kibinafsi.

72 Kuhani wa siku hizo pia atakumbuka waliuza nafasi yao ya kumpata Yeye, nafasi yao ya kuwa mtumishi Wake, kuwa mwanafunzi Wake, kuwa mwongofu Kwake. Waliiuza kwa ajili ya wivu wenye sumu. Walilionea wivu Fundisho Lake. Mbona, wakati alipokuwa na umri wa miaka kumi na miwili tu, angeweza kuwashangaza kwa njia yoyote; na bila kutambua jambo hilo, ya kwamba huyo alikuwa ni Masihi. Hawangeweza kufanya mambo aliyofanya. Nao walihofu kwamba wangepoteza sifa zao mbele ya watu wa hadhi ya juu, nao wakaiuza nafasi yao. Nao wana hatia tu kama Herode alivyokuwa.

73 Na mfuasi wa kanisa leo hii ni vile vile. Kama waliyatumainia madhehebu yao na kadhalika, siku hizo, nao waliogopa ninii yao—hadhi zao kubwa, wangetupwa nje ya masinagogi, ilikuwa ni kitu gani basi? Ilikuwa ni ibada za sanamu! Wakiabudu sanamu za kanuni za imani ama sanamu za kanisa la kidini, badala ya kulikubali Neno lililo hai, ambalo lilidhihirishwa mbele zao.

74 Nao waliliona Neno la Mungu. Biblia ilisema, "Tumemwona na kumpapasa kwa mikono." Wanadamu waliweka mikono yao juu ya Neno halisi la Mungu, lililo hai, lililodhihirishwa; na wakaachilia mapokeo na kanuni za imani zisimame kati yao, kuosha vyungu na sufuria, kitu kichafu jinsi hiyo kisimame kati yao na Mungu aliye hai. Naam.

75 Ilikuwa ni kitu gani? Walimchukia. Waliichukia Injili Yake ya Maandiko iliyo safi kabisa, iliyo dhahiri, aliyokuwa akifundisha, Neno la Baba. Walimwonea wivu. Walimchukia. Na mradi tu wana kumbukumbu, ambapo, wakali kuzimu watakumbuka, hivyo ndivyo watakavyokumbukwa. Hivyo ndivyo itakavyowabidi kumkumbuka.

Unasema, "Loo, hao walikuwa ni Mafarisayo."

76 Kuna maskini mama mmoja aliyezoea kuja kwenye kanisa hili. Loo, ninadhani labda wengi wenu mnamjua, anaishi mbali hapa chini ya mtaa. Alikuwa ameanguka. Na kila nikimwona, ananikimbilia, anaweka mikono yake kwenye yangu, "Ndugu Bill, niombee. Nimerudi nyuma." Mumewe ni ninii . . . La, nafikiri wanaishi upande wa juu wa mtaa huu hapa. Nimemwona katika Roho, nimeiona Roho wa Mungu juu yake, na yeye akicheza, kushangilia, na kadhalika. Naye alikuwa ameanguka. Naye alikuwa amelala hivi majuzi hospitalini hapa nje, akifa, ndivyo walivyodhania. Naye akaniita niende nikamwombee.

77 Yeye na mume wake walikuwa wazuri sana kwa mke wangu, wakati mke wangu, maskini msichana mdogo, mwenye uso mchafu, nguo mbovu, nao wangemnunulia rinda dogo ama kitu fulani mara kwa mara, kumsaidia aende shuleni. Haidhuru ni kitu kidogo jinsi gani, huwezi kumfanyia Mungu jambo moja asiloweza kulikumbuka. "Kadiri mlivyowafanyia walio wadogo wa hawa watoto Wangu, mmenitendea Mimi." Na kama mkate juu ya maji, utarudi.

78 Huyo hapo maskini, mwanamke huyu mdogo, aliyerudi nyuma amelala, analia, akiushika mkono wangu. Na yeye . . . Nikasema, "Vema, dada, nita—nitakuombea."

79 Na kwenye kitanda cha pili kutoka kwake palikuwapo na mwanamke amelala pale na mikono iliyokunjamana, akiniangalia. Na mwanawe mdogo ameketi karibu naye, kadiri ya umri wa miaka ishirini, anayeonekana kama riki wa kisasa.

80 Kwa hiyo, sio kudharau endapo jina la mtu fulani ni Ricky, bali ninamaanisha hiyo ni . . . kamwe hujapata kusikia jina kama hilo katika siku zilizopita. Elvis na Ricky, na ni jina tu la wakati huu, mnaona. Kama una mtoto anayeitwa hivyo, mwite jina lake la katikati, hivyo, ama mpe moja.

81 Ndipo wakati alipokuwa ameketi pale namna hiyo, nikaangalia huko, kisha nikaanza kuinamisha kichwa changu, nami nikamwona ameangalia ninii sana . . . Akasema, "Ngoja kidogo! Rudisha pazia hilo!"

82 Nikasema, "Nilikuwa tu nikitaka kumwombea mama huyu. Hivi—hivi wewe si mwa—mwaminio?"

83 Akasema, "Nitakwambia sasa, sisi ni Wamethodisti, nasi tunakutaka ufunge pazia hilo!"

"Ndiyo, mama," ndipo nikafunga pazia.

84 Mnaona, jambo lile lile. Jambo lile lile siku hizi, kuchukia sana! Alijuaje nilikuwa mhudumu wa aina gani? Sikuwa nimepata kumwona mwanamke huyo. Bali labda alikuwa amemsikia mtu fulani akisema ya kwamba niliamini katika kuponywa kwa wagonjwa, naye alikuwa amefundishwa dhidi yake. Hakuwa na uhusiano wowote nao, alinawa mikono yake kwa huo. Alihofu lingemwangukia. Usiwe na wasiwasi, halitamwangukia, si zaidi ya vile Pilato angaliweza kuliondoa mikononi mwake kwa kulinawa.

85 Sasa, hilo si kusema lolote la kuwatweza Wamethodisti; huyo alikuwa ni mwanamke mmoja tu. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Unaona? Huenda ilikuwa tu ni msimamo wake. Sidhani Wamethodisti wote wangekuwa namna hiyo, maana nimewaombea wengi wao. Wao huniita niwaombee, na ishara na maajabu yamefanywa miongoni mwao. Kamwe si watu kwenye hayo makanisa; ni mfumo walio chini yake, huo ndio unaofanya jambo hilo. Lakini alikuwa mmoja wa aina hiyo. Ilikuwa ni kitu gani? Wivu dhahiri wenye sumu, uliopagawa na ibilisi.

86 Ningeweza kusema jambo fulani. Kwenye—kwenye mkutano fulani uliokuwa hapa jijini wakati mmoja, nao wakauliza ni kwa nini hawakunialika kwenye huo. Lakini nitakwepa hilo kwa sababu niko nyumbani. Lakini, na hata hivyo, hakuna sababu, ni wivu tu, ni kanuni za imani, ni ibada za sanamu. Jinsi ambavyo tungetaka kumkubatia kila mtu, bali wakati unapotengwa . . . Yesu alitaka kufanya jambo hilo. Kumbukeni, siku moja huna budi kukumbuka jambo hilo. Huna budi kulikumbuka.

87 Inanikumbusha tu juu ya ushuhuda uliotolewa hivi majuzi. Mhudumu, naye alikuwa kwenye lifti akipanda juu, hapa kwenye Jengo la Heyburn. Na kulikuwako na watu watatu wamesimama pamoja na mhudumu huyu kwenye—kwenye lifti hiyo, na wao—wao hawakujua mtu huyu alikuwa ni mhudumu, nadhani hawakujua. Basi walipokuwa wakipanda juu, wote walisimama kwenye orofa ya nane. Ndipo mtu mmoja

akamwangalia mhudumu huyo, na akasema, "Unajua nini? Hapa ndipo karibu sana na Mbinguni tutakapopata kufika."

88 "Vema," huyo mhudumu akasema, "Na—nafikiri umesema kweli. Na—nafikiri umesema kweli, kwa kuwa mradi tu tunategemea matendo yetu mema, hatutaenda zaidi ya hapa." Hiyo ni kweli. Mradi tu unategemea yale ufanyayo, unakumbuka yale uliyofanya. Nami nina hakika karibu sisi sote tunajua hatukufanya lolote, hatustahili lolote. Kasema, "Nafikiri kama tunatumainia matendo yetu mema, huu ndio umbali tutakaopata kufika." Vema, kama tunatumainia, huo ndio umbali tutakaofikia.

89 Lakini, loo, ningetaka kusema jambo fulani. Kama ninaweza kusahau kile nilichokuwa, na kukumbuka kile alicho Yeye, kama ninaweza kumkumbuka Yesu, kama ninaweza kumkumbuka pale msalabani, kama ninaweza kukumbuka kile alichonifanyia, na ninaweza kuikumbuka ile saa aliyoziosha dhambi zangu, na kunipa Roho Mtakatifu kuniongoza, basi ninainuliwa juu ya kila kitu kinachoishikilia dunia hii. Ninainuliwa juu ya kila kitu cha duniani, kufikia ulimwengu wa Roho katika Kristo Yesu, ambapo ninaweza kufanya ushirika pamoja na Yeye. Huko katika Uwepo Wake, nikisahau kile nilichopata kuwa, nikisahau dhambi zangu zote na kila kitu, kwa sababu ziko kwenye Bahari ya Usahaulifu. Nikisahau mambo yangu yote ya hapo nyuma, nikisahau kila kitu, na kukumbuka ya kwamba Yeye alinifanya Wake Mwenyewe, kwa mauti Yake Mwenyewe. Alipachukua mahali pangu. Na mimi ambaye sikuwa na haki ya kwenda mahali popote ila jehanamu, Yeye alipachukua mahali pangu na kuniinua kutoka jehanamu. Alienda kule kwa ajili yangu. Naye akaniinua juu kwa wingi wa neema Yake, mpaka sasa sisi ni wana na binti za Mungu, nasi tumeketi kwenye ulimwengu wa Roho katika Kristo Yesu, tukishangilia sikuzote na kumkumbuka Yeye aliyetuleta salama umbali huu. Na tukiwa na imani inayodundadunda mioyoni mwetu, ikitusukuma, na kwa neema yake atanichukua.

90 Na kwa macho ya imani ninayaona Maandiko yake yakitimia, "Wote aliowajua tangu awali, amewaita; wote aliowaita, amewahesabia haki; na wote aliowahesabia haki, amewatukuza." Kwa hiyo kwa wazo hili, ninasimama katika kusanyiko la watu, alipo Roho wa Mungu, nasi tumeinuliwa juu kuketi katika ulimwengu wa Roho katika Kristo Yesu. Tukiutazamia wakati ambao umbo hili potovu la maisha ya kibinadamu ambalo lina kupiga moyo kwa kibinadamu, na ambako hakuna budi kukoma siku moja, ambapo litabadilishwa na kupewa moyo wa Roho utakaodunda katika wakati usio na mwisho ulio bora zaidi ya huo, usio na magonjwa, usio na huzuni, usio na uzee wala chochote.

91 Mkumbukeni Yesu. Wakati lile balasi linapokuwa tupu pale nyumbani, wala hakuna unga mwingine, mkumbuke Yesu.

Wakati daktari anaposema hakuna uwezekano mwingine, mkumbuke Yesu. Wakati ibilisi anapokujaribu; kama tunavyoimba wimbo wetu wa kufumukana, "majaribio yakituzunguka, itia jina hilo katika maombi."

92 Kumkumbuka Yesu, ukikumbuka ya kwamba Yeye atakuja tena. Yesu yeye yule aliyeondolewa kwetu atarudi tena vile vile kama tulivyomwona akipaa Mbinguni. Kumbukeni, Yeye atarudi kwa ajili ya wale walio Wake.

93 Na tuombe, na huku vichwa vyetu vimeinamishwa. Na pamoja na ujumbe huu mdogo uliokatika-katika ukiwa ungali moyoni mwako, je! ungemtaka akukumbuke sasa? Kama ungetaka, inua tu mikono yako, na mambo maalum, "Bwana, nikumbuke." Kama mshairi alivyosema, "Nikumbuke wakati machozi yanapotiririka."

94 Baba yetu Aliye Mtakatifu Sana, tumeufurahia sana Uwepo wa Roho Mtakatifu, jinsi alivyotuonyesha Neno la Uzima, huku tukikumbuka shimo ambalo tulitolewa na sasa tumetolewa kwenye shimo hilo na kufinyangwa tukawa watoto wa Mungu, kwa neema ya Yesu Kristo. Ninamkumbuka, wakati daktari alipoangalia usoni mwangu na kusema, "Ni dakika chache tu zaidi," ninamkumbuka Yesu. Ninamkumbuka Yesu, wakati nilipokuwa madhabahuni nikilia nipate rehema na nafsi yangu ilikuwa imelemewa na mzigo, ninakumbuka mzigo ulioniacha. Yesu aliuchukua mzigo wangu. Miezi michache iliyopita, nikiwa nimeketi kwenye benchi, nikiangalia kwenye darubini ya mtutu wa bunduki, kulenga shabaha, naye Shetani hapana budi aliwazia, "Hii ndiyo nafasi yangu sasa." Na wakati bunduki hiyo ilipolipuka, nao mtutu na tako lake na tendo la bunduki vikarushwa kila upande, nao moto ukaruka ukanizungukia kabisa, na nikajaribu kusimama kwa miguu yangu, nayo damu ikibubujika, ninakumbuka ilikuwa ni Yesu. Wakati daktari, wakati aliponiangalia wala hakuona athari yoyote iliyotokea, yeye alisema, "Jambo pekee nilijualo, ni kwamba hapana shaka Bwana alikuwa ameketi hapo, pia, akimlinda mtumishi Wake, angekuwa amelipuliwa vipande-vipande kwa mlipuko kama huo." Ee Mungu, jinsi sote tunavyoyakumbuka mambo hayo!

95 Tunakuja kwenye chemchemi iliyojaa Damu, iliyotolewa kwenye vena za Imanueli. Tubariki, Bwana, pamoja usiku wa leo. Unajua ku—kusudi na lengo lililo nyuma ya kila moyo ambao umeinua mkono. Wewe unajua shauku na haja. Na kama mtumishi Wako, Bwana, na—naja pamoja nao, na—na juu kutoka kwenye maskani hii sasa (kwa imani) tunaenda, kupita mawingu na mwezi, na nyota na—na kilimia cheupe, na sasa tunafika kwenye Uwepo wa Mungu. Na mbele yangu imetandazwa madhabahu ya dhahabu, hapo pana ile Dhabihu ambayo tunaikumbuka, Yesu, ambaye alisema, "Mwombeni Baba lolote katika Jina Langu, nita—nitalifanya." Jalia imani yetu isishindwe, Bwana, bali jalia tukumbuke

ya kwamba tunapokea tunachoomba, kama tukikiamini, kwa kuwa tunakumbuka Yesu alikufa apate kutupatia hicho na kutuhakikishia.

96 Bwana, tunaona ya kwamba unalipanua jengo letu. Ni Wewe uliyetufanyia jambo hili, ambaye ulitupa upanuzi huu wa kanisa. Nasi tunajua ya kwamba ilikuwa ni Wewe, Bwana, uliyetupa kanisa hili hapo awali. Tunaomba ya kwamba Wewe utabariki jitihada hizi.

97 Bwana, tunamwombea mchungaji wetu, Ndugu Neville, mtumishi wako mnyenyekevu na mwenye fadhili, mwaminifu. Yuko tayari kuhudumu katika hadhi yoyote, haidhuru kama ni kwenye kiti cha nyuma ama kama ni kulifagia kanisa. Popote unapomhitaji, hapo anataka kuwa ni chombo, kukutumikia popote umwitapo. Tunaomba, Mungu, ya—ya kwamba utambariki.

98 Mungu, jaribu hili kuu ambalo ndio kwanza nilipitie, na hawa wadhamini waliosimama pamoja nami, na kanisa hilo ambalo—ambalo liliniombea, na hatimaye ushindi ukaja. Ee Mungu, nawaombea. Ninawakumbuka, pia, Bwana, nami nina hakika Wewe unawakumbuka.

99 Tunakumbuka jinsi umekuwa ni baraka kwetu. Pia tunalikumbuka Neno Lako, ya kwamba kamwe huwezi kutuacha wala kutupungukia. Umri mkubwa hautakuwa na uhusiano wowote nalo, Wewe ungali utatukumbuka, wakati ulimwengu hautakuwako tena na wakati utaishia kwenye umilele. Imeandikwa kitu kama hiki, "Je! mama angeweza kumsahau mtoto wake anyonyaye? Kamwe siwezi kuwasahau. Mmechorwa kwenye vitanga vya mikono Yangu," ile misumari ambayo iliyachora majina yetu. Tunajua ya kwamba Wewe unatukumbuka, Bwana.

100 Na hebu uwe katika kumbukumbu zetu za upendo mwingi sana sikuzote, kama Mwokozi wetu, Mponyaji wetu, Mfalme wetu, Mpenzi wetu, Uzima wetu, Mwanga wetu wa Jua, Yote-katika-Yote kwetu, ile chemchemi isiyoisha ya neema ya Mungu na upendo kwetu sisi wanadamu tulioanguka wa familia ya Adamu. Tujalie, Bwana, tunapojikabidhi Kwako sasa, tukiondoka maskanini usiku wa leo, tukimkumbuka Yesu. Amina.

101 Je! mnamkumbuka? Mnampenda? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Sasa nafikiri, katika Ujumbe wetu mdogo uliovunjika, huenda tukasema jambo hili. Paulo alisema, "Lolote tufanyalo, tulifanye kwa Roho." Katika mambo yote tunapaswa kumkumbuka. Hebu na tusifanye maamuzi mpaka tumkumbuke; hebu tusifanye kitu, maana kitakuwa ni cha kijinga. Kama adui akiupiga upande mmoja wa shavu, hebu na tukumbuke alilofanya kabla hatujampiga. Hebu na tukumbuke tendo Lake. Kama kuna uamuzi wa kufanywa, hebu na

tungoje, tukumbuke aina ya uamuzi ambao tunafikiri Yeye angefanya, halafu tuache huo uwe ndio uamuzi wetu. Kama tukiwa na haraka, hebu na tukumbuke Yeye kamwe hakuwa na haraka. Mnaona? Kama tukishikwa na wasiwasi mkubwa sana, kumbukeni Yeye anaishi katika Umilele, wakati hauna maana Kwake. Ni lengo na kusudi la moyo wetu. Hebu na tumkumbuke.

102 Na hebu tumkumbuke sasa tunapoimba wimbo huu katika Roho wa Uwepo Wake, *Nampenda*. Kama ukidumu katika upendo, unaishi ndani ya Mungu, kwa kuwa Mungu ni upendo. Wale wanaoishi ndani ya Mungu wanaishi katika upendo. Mnaona? Wala upendo hauna chuki. Upendo hauna wivu. Upendo hauna majivuno. Upendo hautendi mabaya. Upendo daima ni mnyenyekevu, mtamu, husamehe, ni mwema. Haidhuru hao wengine wamekasirika vipi, upendo unabaki wenyewe. Upendo ni mkataa wa neema. Upendo ni mkataa wa Mungu kwetu. Baada ya karama zingine zote na kadhalika kutoweka, unabii wetu, ndimi zetu, fasiri zetu, yote tuliyopata kufanya, ama chochote kile, upendo unapoingia, huo ndio mkataa. Umepita vyote, maana mengine yote hushindwa. Ni—ni maamuzi ya Mahakama Kuu. Ni Nguzo ya kufungia. Ni Nyota ya Kaskazini inayowaweka wanamaji sawa. Ni Dira inayotuongoza. Upendo ndio mkataa. Hebu na tukumbuke jambo hilo tunapoimba, "Nampenda."

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

Nampenda, nampenda
Kwani kwanza . . .

Sasa kumbukeni, "Yeye alinipenda, Naye akamtoa Mwanawe."

Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

103 Sasa wakati dada yetu akituchezea wimbo huu, [Ndugu Branham anaanza kuuvumisha *Nampenda*—Mh.] hebu tu katika utamu wa ushirika, wakati tumeketi pamoja katika ulimwengu wa Roho katika Kristo, sasa tuchukue kila kitu, kila kitu kutoka moyoni mwako. Pia kumbukeni, Neno la Mungu linasema hivyo. Mimi ni mtumishi Wake. Yeye yupo hapa. Basi hebu na tupeane tu mikono na mtu fulani, na kusema, "Mungu akubariki, ndugu." Endapo una adui, simama na umwendee, unaona, "Mungu akubariki, ndugu," tunapoimba pambio hilo tena na kupeana mikono sisi kwa sisi. Hivi hutafanya jambo hilo sasa, kwa utamu kweli katika Roho.

Nampenda, (Mungu akubariki, Ndugu Roy) . . .
mpenda
Kwani . . . nipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu

[Ndugu Branham anapeana mikono.] . . .?. . . Huku mikono yetu imeinuliwa sasa.

Nampenda, nampenda
Kwani . . . (Mkumbuke Yesu!)
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

104 Sasa hebu na tuinamishe vichwa vyetu na kuuvumisha. [Ndugu Branham anaanza kuvumisha *Nampenda*—Mh.] Kumkumbuka Yesu! [Ndugu Branham anaendelea kuuvumisha.]

Alinipenda kwanza.

[Ndugu Branham anaendelea kuuvumisha.]

105 Sasa huku dada yetu akiucheza, kwa utamu na polepole, nitamwomba ndugu yetu mwema . . . Ndugu Neville, je! una neno unalotaka kusema, lolote? Vema. Nitamwomba Ndugu Collins huko nyuma, maskini ndugu yetu hapa, mwaminifu, mmoja wa washiriki wenzetu, kama angeweza kuturuhusu tuondoke katika maombi. Wakati tukiinamisha vichwa vyetu, Ndugu Collins.

KUMKUMBUKA BWANA SWA62-1209
(Remembering The Lord)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili jioni, tarehe 9 Desemba, 1962, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani. umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2015 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org